

Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 02 Issue: 01 | Sept-2023

EAJK

# Vigezo vya Utoaji Majina ya Asili ya Watu katika Jamiilugha ya Wagogo

**Authors**
**Jemima Lenjima[(1)]; Jacob Leopold Mwalongo[(2)]**
**Main author email:** lenjimajemima7@gmail.com

**(1.2) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**Cite this article in APA**
Lenjima, J., & Mwalongo, J. L. (2023). Vigezo vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, 2(1), 107-116. https://doi.org/10.51317/eajk.v2i1.398

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 29.07.2023
Accepted: 31.08.2023
Published: 11.09.2023

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2023 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Makala haya yamejikita katika kuchunguza vigezo vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo. Makala haya yameongozwa na swali moja katika kuandaliwa kwake. Swali hilo linauliza: Vigezo gani vinavyotumika katika utoaji wa majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo? Mbali na kujadili swali hilo muhimu, makala pia yametoa mapendekezo kuhusu njia za kuendeleza matumizi ya majina ya asili ya watu katika jamiilugha husika. Makala haya ni muhimu kwa watu wote yaani wanaotumia majina ya asili ya watu na wasiotumia majina hayo. Data ambayo ilichunguzwa ni sehemu ya data iliyokusanywa kutoka katika wilaya ya Mpwapwa na Chamwino kutoka katika mkoa wa Dodoma nchini Tanzania. Vijiji vya Mima na Gulwe kutoka wilaya ya Mpwapwa na vijiji vya Mvumi Misheni na Handali kutoka wilaya ya Chamwino vimehusishwa. Uchanganuzi na uchambuzi wa data za makala haya umetumia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa katika kukusanya data uwandani na umeongozwa na Nadharia ya Uumbaji ya Sapir- Whorf (1958) inayosisitiza kwamba lugha ndio msingi wa kuuelewa ulimwengu. Mtu anapojifunza lugha ni kama anatawaliwa na lugha hiyo hata dunia unayoiumba akilini mwako itatokana na dunia ilivyoratibiwa na wasemaji wake. Katika kuchambua na kuwasilisha data, makala haya yametumia mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya uchunguzi yamedhihirisha vigezo mbalimbali vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo. Vigezo hivyo huweza kuwa na mfanano katika mambo fulani na wakati huohuo kunaweza kuwa na upekee unaotafautisha jamiilugha moja na nyingine.

**Maneno muhimu:** Jamiilugha, Jina, Majina Ya Asili, Vigezo, Wagogo.

**UTANGULIZI**

Kila kiumbe na hali zote majina hupewa na binadamu ili kusaidia utambuzi wa haraka wa kile kinachorejelewa. Utoaji wa majina ya watu katika jamii nyingi za Kiafrika haufanyiki kiholela bali huzingatia vigezo, taratibu na kanuni fulani zilizobeba maana kulingana na mila na desturi za jamii hiyo. Katika jamii nyingi za Kiafrika na duniani kote kwa ujumla, majina ni muhimu sana. Jina ni zaidi ya neno linalomtambulisha mtu mmoja na mwingine. Matsimela (1997) alisema kuwa, huko nyuma katika jamii nyingi za Kiafrika, mtoto alipozaliwa alipewa jina kwa kufuata kanuni na taratibu fulani zinazotofautiana toka kabila moja na jingine kulingana na mila na deasturi za watu wa jamii alipozaliwa mtoto huyo. Hii ni kwa sababu jina la jamii fulani hufungamana na imani fulani ambayo huambatana na mila na desturi za utamaduni wa jamii husika.

Mbiti (1990) alisema kuwa, katika imani za asili za kiafrika, majina yana athari katika maendeleo ya mtoto ya baadaye. Mawazo ya Mbiti yaliungwa mkono na Koigi (2008), Rugemalira (2005), Matsimela (ameshatajwa) na Rey (1995) waliposema kuwa, jina husaidia katika utambuzi wa mtu kibinafsi na kirasmi, kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. Pia, jina hilo hilo humtambulisha mtu eneo analotoka, huashiria tabia yake, sifa zake, imani na fikra zake. Hata hivyo, hivi sasa utamaduni huu wa kuita majina watoto majina ya asili, ambao umetoweka kwa wengi. Katika jamiilugha ya Wagogo watoto wengi wamekuwa wakipewa majina yasiyo ya asili huku majina ya asili yakiachwa na kupuuzwa kutokana na ujio wa vitu anuai. Rugemalira (2005) katika utafiti wake alisema kuwa, majina na lugha nyingi za kibantu zinafifia na hata kuwa hatarini kupotea au kutoweka kutokana na watu hasa vijana kutojua thamani iliyobebwa na majina ya lugha hizo hasa katika utambulisho wao katika nyanja mbalimbali.

Lengo kuu la makala haya yameongozwa na swali moja katika kuandaliwa kwake. Swali hilo ni vigezo gani vinavyotumika katika utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo? Ili jamii hiyo iweze kuenzi, kulinda na kudumisha majina hayo katika jamii yao na jamiilugha mbalimbali katika makabila ya Tanzania na duniani kote kwa ujumla.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Malande (2011) alifanya utafiti kuhusu maana za majina ya watu wa kabila la Lulogooli lililopo magharibi ya Kenya na aligundua kuwa kuna mikabala miwili ya kimaana katika majina ya watu katika kabila la Lulogooli yaani mkabala wa maana halisi na mkabala wa maana kimaibala. Alitoa mfano wa jina Ambura ambalo aliitwa mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati kilikuwa kunanyesha na jina Imburani hitwa mtoto wa kike aliyezaliwa wakati wa mvua. Utafiti huu umekuwa chachu katika kuandaa makala haya kwani umesaidia kuonesha kigezo kinachotokana na matukio ya msimu au vipindi mbalimbali kinachotumika katika utoaji wa majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo.

Kofi (2006) alitafiti majina ya watu wa kabila la Akani nchini Ghana aligundua kuwa watu wa kabila la Akan huwapa watoto wao majina kulingana na siku ya kuzaliwa, familia aliyozaliwa, tukio la tohara (jando), athari za kimaumbile, majina yanayotokana na mafanikio, kama watoto wamezaliwa pacha, dini, majina ya kimiujiza,, majina ya vijembe na methali (mafumbo), majina ya umbo la mtoto la mtoto aliyezaliwa na majina ya ukoo. Kofi (ameshatajwa) anaeleza kuwa, Waakani wanaamini kuwa jina linalofungamana na nguvu za asili hutarajiwa kuwa kielelezo na kiwakilishi hasi au chanya cha maisha na tabia za watu.

Guma (2001) alifanya utafiti wa majina ya watu katika jamii ya Basotho kule Afrika ya Kusini. Kutokana na utafiti huo, alibaini kuwa jina ni zaidi ya neno au maneno yanayomtambulisha mtu. Aliendelea kusema utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni linaloonesha historia ya jamii. Anaendelea kusema kuwa majina husimamia desturi, tajiriba ya mtu au kikundi cha watu, mila, hadhi na mamlaka katika jamii. Ingawa utafiti huu hauhusiki na majina kama utambulisho lakini utafiti wa mtalaamu huyu umekuwa msaada mkubwa katika makala haya, kwa sababu utafiti huu pia ulichunguza majina ya watu katika jamii ya Basotho tofauti na makala haya yanayochunguza vigezo vya utoaji majina ya watu katika jamiilugha ya Wagogo.

Chulk (1992) alitafiti majina ya watu wa Afrika ambapo alieleza kuwa watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, vitu vikubwa vya kushangaza, siku ya

juma mtu alipozaliwa. Mfano "Ainde" Kiyoruba lina maana ya tuliyekuwa tumemuomba au tunamsubiri. Jina hili limetokana na familia ambayo kwa muda mrefu haijapata mtoto wa kiume.

Sinani (2018) katika utafiti wake uliohusu tathimini ya maana na vigezo vilivyotumika katika kutoa majina ya utani katika jamii ya Wapemba. Utafiti wake ulibaini kuwa majina ya utani hayatolewi kiholela bali kuna vishawishi ambavyo huchochea uibukaji wa majina hayo ambayo huakisi masuala mbalimbali ya kijamii kama vile shughuli za mhusika binafsi, matukio ya kihistoria, urithi kutoka kwa wazazi, umbile la mhusika na visa au matukio anayoyafanya mhusika. Hivyo basi, matokeo ya utafiti wake yamedhihirisha kuwa majina ya utani hufungamana na jamii husika.

Resani (2017) alichunguza maana na asili ya majina ya watu katika jamii ya Wabena. Jina kulingana na Plato ni aina ya maneno na njia pekee ya kurejelea dhana au kitu. Maana ilihusishwa na jina na ujinaishaji (Resani, 2015). Kutokana na umuhimu wa jina binadamu wamepewa na kupeana majina kama kitambulisho cha kuwatambulisha miongoni mwa jamii husika. Kila jamiilugha ina majina ambayo hutambulisha zaidi ukweli unabaki kuwa kila jina apewalo mtu lina maana na athari kwa muhusika. Matokeo ya uchunguzi wake yalionesha kuwa maana inayopatikana katika majina mengi katika jamii ya Wabena hutokana na wasifu wa mwenye jina. Mathalani wakulima hodari, wawindaji hodari, matajiri wakubwa na watawala wa jadi (machifu), wahunzi wazuri. Vilevile, kuna huwezekano wa kurithi majina ya ndugu zao walio hai au waliokwishafariki, lengo ni kutunza kumbukumbu za ndugu hao.

Samwel (2016) utafiti wake ulihusu utaratibu wa utoaji wa majina ya asili na maana zake katika jamii ya Wamasai wanaoishi Arusha vijijini mkoa wa Arusha Tanzania. Utafiti huu umebainisha kuwa mazingira ya makutano yanajidhihirisha katika jamii ya Kimasai kuendelea kutoa majina ya rika kwa kuzingatia matukio ya kihistoria. Pia utafiti huu umebaini kuwa katika jamii ya Wamasai majina ya rika huweza kupewa jina jipya. Utoaji wa majina ya rika kwa rika kwa kila hatua husaidia kuhimiza majukumu ya jamii na mipaka ya kila rika ili kudumisha heshima na uwajibikaji katika jamii. Vilevile, majina ya utani wa rika hutumika zaidi ili kutimiza historia ya jamii hiyo. Aidha, utaratibu wa utoaji wa majina ya ukoo ni wa kurithishana isipokuwa mtu aliruhusiwa kubadili jina la ukoo kwa utaratibu wa kubadili chapa na alama kwenye masikio ya ng'ombe, mbuzi au kondoo pamoja na kunyolewa nywele ili kuashiria kuachana na jina la awali.

Abel (2012) yeye alichunguza matumizi ya majina ya ukoo katika utambulisho wa jamii ya Wasambaa. Katika utafiti huo aliweza kubainiha maumbo ya majina ya ukoo jinsi yanavyotambulisha jamii ya Wasambaa na kueleza asili na maana ya majina hayo ya ukoo. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa maana za majina ya Kasambaa hutolewa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama vile matukio ya jamii, tabia za watu, mabadiliko ya tabianchi, shughuli za kijamii na kiutawala, utani, mtu alikozaliwa na majina yatokanayona na majina ya wanyama na mimea.

**MBINU ZA UTAFITI**

Data za makala haya zilikusanywa uwandani katika mkoa wa Dodoma, wilaya ya Mpwapwa na Chamwino. Vijiji vilivyohusishwa ni Mima na Gulwe kutoka wilaya ya Mpwapwa na Mvumi Misheni na Handali kutoka wilaya ya Chamwino, kwa kutumia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa. Jumla ya watoataarifa arobaini na nane (48) waliteuliwa kimakusudi, yaani watoataarifa kumi na mbili (12) kutoka kila kijiji, kwa kuzingatia umahiri wa lugha ya Kiswahili na Kigogo pamoja na jinsi. Kigezo cha jinsi kimetumika kwa sababu katika jamiilugha ya Wagogo baba na mama ndio wanaohusika katika kutoa jina kwa mtoto anayezaliwa. Makala haya yametumia mkabala wa kitaamuli (maelezo) na Nadharia ya Uumbaji imetumika pia katika uchambuzi wa data.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Kipengele kilichojadiliwa katika uchunguzi wa mada ya makala haya ni vigezo vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo na mapendekezo kwa ujumla.

**Vigezo vya Utoaji Majina ya Asili ya Watu Katika Jamiilugha ya Wagogo**

Katika kukamilisha lengo la makala haya ambalo ni kubainisha vigezo vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo, makala yamedhihirisha vigezo vifuatavyo ambavyo ni kigezo cha matukio,

tabia na matendo ya watu, mahali pa kuzaliwa, majina ya ujio wa vitu vipya, majina ya wanyama, ndege na wadudu, mahusiano katika familia, kigezo cha hali ya kipato cha familia na kigezo cha namna mtoto alivyozaliwa. Hebu tuangalie vigezo hivyo kama ifuatavyo:

**Kigezo cha Matukio**

Matukio ni mambo yote yanayojiri katika jamii. Matukio hayo yanaweza kuwa furaha ama huzuni. Katika jamiilugha ya Wagogo hutoa majina ya asili kwa kutumia vigezo vinavyotokana na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii yao kama vile matukio ya vita, matukio ya majanga, matukio ya Mungu pamoja na matukio ya vipindi au misimu mbalimbali. Matukio hayo ndani yake hubeba kumbukumbu muhimu katika jamii husika. Dai hili linaungwa mkono na Tegisi (2019) alipotafiti majina ya asili katika koo za Ginantuzu alieleza kuwa majina yanayotokana na matukio fulani hubeba kumbukumbu katika jamii. Tazama hapa chini ufafanuzi wa baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo yanatokana na kigezo cha matukio mbalimbali.

1. ***Mlekwa*** (yatima): Jina hili hupewa mtoto wa kike au wa kiume ambaye amezaliwa na kukuta wazazi wote wamefariki au amezaliwa baada ya kipindi kifupi tu kabla ya kupewa jina akaachwa na wazazi wake wote na kubaki yatima. Hivyo walezi waliobaki hulazimika kumpa jina la ‘***Mlekwa’*** na‘***Kalekwa’*** maana yake yatima ameachwa baada ya wazazi wake wote kufariki.

2. ***Lyadumka*** (yatima): Jina hili hupewa mtoto ambaye wazazi au mzazi mmoja alifarika kabla au baada ya mtoto kuzaliwa. Jina hili hupewa mtoto wa kike au wa kiume kwa ajili ya kutunza kumbukumbu kwa familia husika kuhusiana na tukio hilo namna lilivyotokea.

3. ***Manzije*** (nzige): Jina hili hutolewa kwa mtoto wa kike au wa kiume ambaye huitwa ‘***Nzije’*** aliyezaliwa wakati wa tukio la balaa la nzige. Majina haya hutolewa katika jamiilugha ya Wagogo kwa baadhi ya watoto wao kwa kuweka kumbukumbu ya tukio husika hapo baadaye. Kama majina mengine yalivyo, si watoto wote hupewa majina hayo wakati wa tukio husika bali wengine hupewa majina hayo kulingana na upendeleo wa wazazi wao hata kama tukio hilo halipo kwa wakati huo.

4. ***Mamvula*** (mvua): Jina hili hupewa mtoto wa kike ambaye alizaliwa katika msimu wa mvua au mwaka uliokuwa na mvua nyingi ambayo iliweza kuiathiri jamii katika sehemu husika. 'Matonya' ni jina alilopewa mtoto wa kiume aliyezaliwa katika kipindi cha mvua. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa na mtafiti uwandani walieleza kuwa, majina hayo hutolewa kwa watoto hata kama hakuna tukio la mvua kwa kurithi jina hilo kutoka kwa ndugu au jamaa wa karbu na familia ili kuweka kumbukumbu kwa jamii husika kwa ajili ya tukio la mvua.

5. ***Mazengo*** (miti ya kujengea): Jina hili hupewa mtoto wa kiume ambaye alizaliwa wakati wa kuandaa miti ya kujengea nyumba ama alizaliwa sehemu ambayo miti hii ya kujengea nyumba imekusanywa na kuhifadhiwa. Kwa mujibu wa watoataarifa walieleza kuwa hapo zamani nyumba zote za jamiilugha ya Wagogo zilijengwa kwa kutumia miti hakukuwa na matofali ya udongo wala saruji. Majina mengine ni ‘***Nzengo’***, na ‘***Izengo***.

**Kigezo cha Tabia na Matendo ya Watu**

Majina ya asili ya watu yanayotokana na kigezo cha tabia na matendo ya watu kwa kawaida huakisi mienendo ya wahusika. Mienendo hiyo hujumuisha ukarimu, upendo, upole, ukali, ulevi, hasira, wema ama ubishi. Tabia na matendo hutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine. Anusa (2016) anaeleza katika utafiti wake kuwa, majina ambayo yanatokana na tabia kimsingi huakisi mienendo ya wahusika. Makala haya yamebaini kuwa katika jamiilugha ya Wagogo kuna baadhi ya majina ya watu ya asili yatokanayo na tabia na matendo ya watu. Hebu tuangalie hapa chini ufafanuzi wa baadhi ya majina ya asili ya watu yanayotokana na kigezo cha tabia na matendo ya watu.

1. ***Udoba*** (mvivu): Jina hili hupewa mtoto wa kiume ambaye mama yake alikuwa na tabia ya uvivu wakati wa ujauzito wake. Wakati mwingine wazazi wa mtoto huamua kumpa

mtoto wao jina hilo kwa kurithi jina la mwanzilishi wa jina hilo ambaye anaweza kuwa mzazi mmoja au ndugu wa karibu ili asije akarithi tabia ya uvivu. Pia kutunza kumbukumbu ya mwanzilishi wa jina hilo lisije likapotea.

2. ***Kuhodanga*** (kuharibu): Jina hili hupewa mtoto wa kiume kwa kurithi kutoka kwa wazazi au ndugu wa karibu. Ili kuweka kumbukumbu lisipotee. Pia, jina hili hutolewa na wazazi wakati mama akiwa mjamzito au baada ya kujifungua mzazi mmojawapo akiwa na tabia ya kuharibu vitu au mambo fulani katika familia..

3. ***Wendo*** (upendo): Hili ni jina ambalo hupewa mtoto wa kike linaloashiria upendo baina ya wazazi au familia ama jamii husika. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa kwa njia ya mahojiano na majidailiano ya kundi lengwa, walieleza kuwa jina la '*Wendo*' hutolewa kwa mtoto ambaye wazazi wake wana tabia ya kuonesha upendo kwa watu wengine. Pia, hutolewa na wazazi ambao familia yao ina amani hasa baba na mama kipindi cha ujauzito wa mama kama wazazi walioneshatabia ya upendo basi mtoto baada ya kuzaliwa huitwa jina hilo.

4. ***Chipegwa*** (pewa): Hili ni jina ambalo hupewa mtoto wa kike baada ya kuzaliwa kwa kurithi kutoka kwa mwanzilishi au kutoka kwa wazazi wake. Jina la '*Chipegwa*'hutolewa na wazazi ambao huenda walitafuta mtoto kwa muda mrefu bila mafanikio na baada ya muda mrefu wakafanikiwa hivyo wazazi humpa mtoto huyo jina hilo. Pia, jina hilo huweza kupewa mtoto kwa kurithi kutoka kwa mwanzilishi ambaye ni ndugu wa karibu ili kuweka kumbukumbu ya jina hilo lisipotee.

5. ***Maseko*** (cheko): Jina hili hupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati wazazi wana amani na furaha kiasi kwamba kuzaliwa kwa mtoto huyo kulileta kicheko na furaha ndani ya familia na jamii kwa ujumla. Jina hili pia huweza kupewa mtoto kwa kurithi kutoka kwa mwanzilishi ndugu wa karibu wa familia hiyo ili kuweka kumbumbu lisipotee na kwa mtoto wa kike huitwa '*Seche*'.

**Kigezo cha Mahali pa Kuzaliwa**

Mahali pa kuzaliwa ni kigezo kimojawapo kinachotumika katika kutolea majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo. Hata hivyo watoataarifa waliofikiwa na mtafiti kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na nadharia ya Sapir- Whorf (1958) walieleza kuwa, majina ya asili ya watu yanayotokana na kigezo cha mahali pa kuzaliwa baadhi hayatokani na mahali alipozaliwa mtoto bali yanatokana na kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu yao. Wengine hujiita wenyewe wakisha kuwa wakubwa kulingana na kupenda mahali fulani. Hebu tuangalie ufafanuzi wa baadhi ya majina haya kama ifuatavyo hapa chini:

1. ***Madeha*** (nje): Jina hili kutolewa kwa mtoto wa kiume ambaye amezaliwa nje ya mazingira ya nyumbani kama vile shambani au sehemu nyingine. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa walieleza kuwa jina la '*Madeha*' pia hupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa nje ya ndoa.

2. ***Ibago*** (pori): Jina hili hupewa mtoto wa kiume ambaye mama yake alishikwa uchungu akiwa porini katika shughuli mbalimbali kama vile kukatakuni ama kutafuta mboga na kujifungulia huko au kupelekwa hospitali lakini uchungu aliugulia porini. Kwa mujibu wa watoataarifa walieleza kuwa jina la '*Ibago*', '*Chibago*' na '*Libago*' hutolewa kwa mtoto wa kiume wakati baba wa mtoto akiwa machungani au mawindoni alimuacha mama wa mtoto akiwa na ujauzito na kujifungua mtoto baba wa mtoto akiwa bado yuko porini.

3. ***Chitunda*** (kilima kidogo): Ni jina ambalo hutolewa kwa mtoto wa kiume aliyezaliwa mama yake akiwa mlimani katika shughuli ya kuokota kuni, kutafuta dawa na shughuli nyingine.Akiwa huko uchungu alikutwa na uchungu na kujifungulia huko. Pia ni jina ambalo hutolewa wakati mama akiwa mjamzito na baba wa mtoto akiwa mlimani

kwa ajili ya shughuli za uwindaji au ulishaji wa mifugo huku mama alijifungua mtoto yeye baba akiwa mlimani mtoto hupewa jina la '*Chitunda*'au '*Matunda*'.

4. ***Nyamiti*** (dawa): Jina hili hupewa mtoto wa kike na wazaziwake wakati mama akiwa mjamzito alikwenda kutafuta dawa porini, akiwa huko alipatwa na uchungu. Kwa mujibu wa watoatoataarifa walieleza kwamba, jina la '*Nyamiti*' hutolewa kwa mtoto wa kike ambaye wazazi walitafuta mtoto kwa muda mrefu sana baadaye wazazi walitafuta dawa na kutumia hizo dawa ndipo akapatikana mtoto huyo. Vile vile jina hilo hupewa mtoto kwa kurithi kutoka kwa mwanzilishi ili kuweka kumbukumbu na lisipotee.

5. ***Chiligati*** (tumo ndani): Jina hili hupewa mtoto wa kiume ambaye baba na mama wa mtoto wakati wa ujauzito alipatwa na uchungu na kujifungulia mtoto ndani bila kupelekwa hospitalini wakiwepo wazazi wote wa mtoto. Mtoto hupewa jina hilo ili kusadifu mazingira halisi kwa ajili ya kumbukumbu.

**Kigezo cha Majina ya Ujio wa Vitu Vipya**

Majina ya asili ya watu yanayotolewa kwa kigezo cha majina ya ujio wa vitu vipya yanatolewa kwa watoto wadogo na mengine hutolewa kulingana na athari ya kitu hicho kwa watu wazima katika jamii husika. Majina haya hutolewa kwa watu kutokana na ujio wa vitu vipya au utawala mpya ambao hapo mwanzo haukuwepo kwa jamii husika. Lengo la kuwapatia watoto majina hayo, ni kuweka kumbukumbu kwa jamii juu ya ujio wa vitu hivyo au utawala, Ufafanuzi wa baadhi ya majina ni kama ifuatavyo:

1. ***Itelejita*** (trekta): Jina hili alipewa mtoto wa kiume ambaye alizaliwa kipindi cha ujio wa trekta. Ujio wa chombo hiki cha kilimo mwanzoni kiliwashangaza sana jamiilugha ya Wagogo kwa utendaji kazi wake kwani trekta liliweza kulima hata kwenye sehemu ya ardhi iliyoshindikana. Kutokana na ujio wa chombo hiki Watoto waliozaliwa kipindi hiki walipewa jina hilo kama ukumbusho. Jina la '*Itelejita*' halikutolewa kwa Watoto tu hata watu wazima walijiita wenyewe au kuitwa na watu wengine kutokana na utendaji wao wa kazi.

2. ***Ndejeulaya*** (ndege ya abiria): Jina ambalo hupewa mtoto wa kiume baada ya kuzaliwa kutokana na ujio wa ndege ya abiria. Jina la '*Ndejeulaya*' kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa na mtafiti kwa njia ya mahojiano na kundi lenwa kwa kuongiozwa na nadharia ya Uumbaji walieleza kuwa, mtoto aliweza kupewa jina hilo kwa sababu alizaliwa kipindi au wakati wa ujio wa ndege za abiria. Jina hilo hutolewa kwa mtoto au muhusika kujiita mwenyewe ili kuweka kumbukumbu tu wakati wa ujio wa ndege hizo.

3. ***Mkapa*** (Rais wa awamu ya tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania): Jina hili hupewa mttoto wa kiume baada ya kuzaliwa katika kipindi cha utawala wa Rais Magufuli. Kwa mujibu wa watoataarifa walieleza kuwa, waliamua kuwapa watoto wao jina hilo wakiwa na imani kuwa watoto wao baada ya kukua watakuwa viongozi wenye tabia na ujasiri kama aliyokuwa nayo Rais wa awamu ya tatu. Pia kuweka kumbukumbu kwa ajili ya jamii husika.

4. ***Mapogo*** (bangili): Jina hili hupewa mtoto wa kike na wazazi wake baada ya kuzaliwa katika kipindi cha ujio wa bangili. Jina hili hutolewa kama ukumbusho kwa jamii husika pia kwa kurihi kwa mwanzilishi wa jina hilo ambaye ni ndugu wakaribu katika familia husika.

5. ***Mapesa*** (mtu mwenye pesa/ asiye na pesa): Jina hili hupewa mtoto wa kiume ambaye wakati wa kuzaliwa kwake wazazi wake walikuwa na pesa nyingi au kipindi mtoto huyo anazaliwa wazazi wake hawakuwa na pesa kabisa waliishi maisha ya shida. Pia jina hilo hutolewa kwa mtoto kutokana na kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu ili kuweka kumbukumbu jina hilo lisipotee kwa jamii husika.

**Kigezo cha Majina ya Wanyama, Ndege na Wadudu**

Kundi hili la majina ya asili ya watu yanayotokana na kigezo cha majina ya wanyama na ndege wanaopatikana katika mazingira ya jamii husika. Kutokana na maelezo yaliyotolewa na watoataarifa kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa, imedhihirika kuwa kigezo cha majina ya wanyama, ndege na wadudu ni kigezo kinachotumika katika utoaji wa majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo:

1. ***Puma*** (nyani): Jina hili hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ikiwa mama wa mtoto huyo akiwa mjamzito au wakati wa alijifungua wanyama hao walipatikana kwa wingi katika mazingira yao. Watoataarifa walieleza kwamba, jina hilo aliweza kupewa mtoto husika kutokana na athari yoyote iliyotokana na wanyama hao kipindi mama wa mtoto huyo akiwa mjamzito au wakati wa kuzzaliwa. Pia jina hilo hutolewa kwa mtoto kwa kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu ili kuweka kumbukumbu lisipotee.

2. ***Manzije*** (nzige): Jina hili alipewa mtoto wa kike na wa kiume aliitwa '*Nzije*' ikiwa mtoto huyo alizaliwa kipindi cha ujio wa nzige kama kumbukumbu kwa wazazi, familia na jamii katika ujio wa balaa la nzige kwa kipindi husika. Jina hilo lilitolewa kutoka na athari zilizotokana na wadudu hao katika jamii husika.

3. ***Nghwezi*** (aina ya ndege tausi): Jina ambalo hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ambaye mama yake wakati wa ujauzito au kujifungua alikuwa ni kipindi cha upatikanaji wa ndege tausi wengi. Hivyo, watoto waliozaliwa wa kiume waliozaliwa kipindi hicho walipewa jina la *Nghwezi* na watoto wa kike waliitwa *Nyanghwezi*.

4. ***Mmehe*** (mchwa): Jina hili hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ambaye alizaliwa katika kipindi mchwa walijitokeza kwa wingi na kuleta athari hasa katika mazao shambani na kusababisha mazao mengi kuanguka hasa baada ya kuliwa na mchwa. Hivyo, jina hili hutolewa kwa mtoto wa kiume na wa kike hupewa jina la '*Chimmehe*'.

5. ***Samamba*** (mbayuwayu): Jina hili hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ambaye alizaliwa kutokana na ujio wa ndege hawa kwa wingi katika eneo husika. Licha ya kupatikana kwa wingi ndege hao jina hilo pia alipewa mtoto kutokana na athari yoyote iliyofanywa na ndege hao kipindi mtoto huyo anazaliwa.

**Kigezo cha Mahusiano katika Familia**

Mahusiano katika familia ni mojawapo ya kigezo kingine kinachozingatiwa katika utoaji majina kwa jamiilugha ya Wagogo. Mahusiano yanaweza kuwa mazuri au mabaya katika jamii au familia husika. Majina haya hueleza mahusiano halisi yaliyo katika jamii au familia husika kwa ujumla. Majina haya yanaweza kuwa na nia ya kueleza hali ya upendo, amani, furaha, huzuni, chuki, ugomvi na migogoro katika familia husika. Ufuatao hapa chini ni ufafanuzi wa baadhi ya majina hayo.

1. ***Nhanwa*** (kataliwa): Hili ni jina analopewa mtoto wa kiume na wazazi wake, ndugu wa karibu au jamii yake baada ya mtoto au mama wa mtoto wakati wa ujauzito au kujifungua kukataliwa na baba wa mtoto baada ya kuzaliwa au kabla ya kuzaliwa baba wa mtoto akiamini kuwa mtoto aliyezaliwa au mimba siyo ya kwake. Jina hilo pia hupewa mtoto kutokana na kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu sana ili kutunza kumbukumbu.

2. ***Mbezwa*** (fukuzwa): Jina hili hupewa mtoto ambaye mama yake alifukuzwa na baba wa mtoto au familia kabla au baada ya mtoto kuzaliwa. Jina ambalo hutolewa na wazazi wa mtoto huyo kutokana na vurugu au ugomvi uliojitokeza katika familia hiyo kama kumbukumbu ya tukio hilo. Jina hilo pia hutolewa kwa mtoto hata kama hakuna tukio hilo, kutokana na kurithi jina hilo kutoka kwa ndugu wa karibu wa familia hiyo.

3. ***Seche*** (kicheko): Jina hili hupewa mtoto wa kike na wazazi wake ambaye mama wa mtoto kabla au baada ya kuzaliwa mtoto huyo kilikuwa ni kipindi ambacho wazazi walikuwa

na amani, upendo na furaha ambayo ilisababisha kicheko ndani ya familia, ndugu na jamii kwa ujumla. Jina hilo hutolewa na wazazi wa mtoto kutokana na kutopata mtoto kwa muda mrefu hivyo baada tu ya kuzaliwa kwa mtoto huleta kicheko kwa familia. Akizaliwa mtoto wa kiume huitwa '*Maseko*'.

4. ***Mtaze*** (saidia): Hili ni jina ambalo hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake aliyezaliwa kipindi mama wa mtoto alikuwa akiomba msaada wakati wa ujauzito wake au kujifungua mtoto huyo. Jina hilo pia hutolewa kwa mtoto kutokana na vurugu au ugomvi wa wazazi wa mtoto huyo au ndugu wa karibu wa familia kabla au baada ya mama wa mtoto huyo kujifungua. Pia jina hilo hutolewa kwa kurithi kutoka kwa mwanzilish au ndugu wa karibu mwenye jina hilo ili kutunza kumbukumbu.

5. ***Mwendwa*** (pendwa): Jina hili hutolewa kwa mtoto wa kike ambaye alizaliwa katika kipindi cha amani na furaha. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa walieleza kwamba, mtoto anapopewa jina hilo humaanisha kuna amani, furaha, upendo na mshikamano katika jamii au familia husika. Pia jina hilo hupewa mtoto kutokana na kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu wa familia husika.

**Kigezo cha Hali na Kipato cha Familia**

Hali na kipato katika familia ni kigezo kingine kilichozingatiwa katika utoaji wa majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo. Matokeo ya makala haya yamedhihirisha kuwa, katika jamiilugha kuna baadhi ya majina ya asili ya watu hutokana na kigezo cha hali ya kipatocha familia. Ufafanuzi wa baadhi haya ni kama ifuatavyo:

1. ***Lyahali*** (masikini): Hili ni jina analopewa mtoto wa kiume au wa kike kutokana na hali ya uchumi duni wa wazazi wa mtoto huyo katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Jina hili hutolewa ili kutunza kumbukumbu kwa familia hapo mbeleni kuwa mtoto huyo alizaliwa wakati familia ilikuwa na hali duni ya kiuchumi..Jina hili pia hutolewa kwa mtoto ambaye wazazi wake wote wawili walifariki akiwa bado mtoto mdogo. Vile vile jina hili hutolewa kwa mtoto kuurithi kwa ndugu wa karibu hata kama familia hiyo kwa wakati huo itakuwa vizuri kiuchumi.

2. ***Lyagaya*** (mateso): Hili ni jina analopewa mtoto wa kike na wa kiume hupewa jina la '*Magayo*' ambaye amezaliwa na kukuta kuna mateso ya kila aina kwenye familia ya mtoto husika. Mateso hayo yanaweza kuwa hali duni ya kiuchumi ya kifamilia au kijamii. Jina hili pia wakati mwingine hutolewa kwa mtoto aliyezaliwa kama jina la urithi kutoka kwa mwanzilishi wa jina hilo hata kama hali ya mateso haipo tena kwenye familia yao hii ni kutunza kumbukumbu ili jina hilo lisipotee.

3. ***Mang'ombe*** (ngombe wengi): Jina hili hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ambapo mama kabla au wakati wa kujifungua alikutana na ng'ombe wengi wakiwa wanakwenda machungani. Pia jina hilo hutolewa kwa mtoto aliyezaliwa katika familia ya wafugaji wakubwa wa ng'ombe kama utambulisho wa utajiri kwa familia husika. Jina hilo pia hupewa mtoto kama ishara ya kumtakia maisha bora ya baadaye. Kwani katika jamiilugha ya Wagogo ni wafugaji hivyo kuwa na ng'ombe wengi ni ishara ya kuwa na uchumi mzuri.

4. **Wanjiye** (pungukiwa): Hili ni jina analopewa mtoto wa kiume ambaye alizaliwa wakati au kipindi ambacho wazazi wake walikuwa wamepungukiwa kiuchumi na kusababisha kuishi maisha magumu. Wakati mwingine jina hilo hutolewa kwa mtoto kama jina la urithi kwa mwanzilishi wa jina hilo ili kuweka kumbumkumbu lisipotee.

**Kigezo cha Namna Mtoto Alivyozaliwa**

Katika jamiilugha ya Wagogo kuna baadhi ya majina ya asili ya watu yalitolewa kwa waanzilishi wake kutokana na kigezo cha jinsi au namna mtoto alivyozaliwa. Matokeo ya makala haya yamebaini kuwa katika jamiilugha ya Wagogo majina haya hujumuisha afya ya mtoto, kuzaliwa kusiko kwa kawaida, kutelekezwa

kwa mtoto baadaau kabla ya kuzaliwa, rangi ya mtoto na namna nyinginezo. Hebu tuangalie ufafanuzi wa baadhi ya majina hayo hapa chini:

1. ***Chilongozi*** (kitangulizi): Hili ni jina hupewa mtoto wa kiume na wazazi wake ambaye kwanza kwanza kuzaliwa au kifungua mimba kwa familia. Wakati mwingine jina hutolewa kwa mtoto aliyezaliwa kwa kurithi jina hilo kutoka kwa mwanzilishi wa jina hilo ili kuweka kumbukumbu kwa familia husika.

2. ***Mziwanda*** (mtoto wa mwisho): Mtoto wa kiume au wa kike hupewa jina hili na wazazi wake au ndugu wa karibu kwa mtoto ambaye amezaliwa mwisho katika tumbo la mama yake. Watoataarifa waliofikiwa na mtafiti kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na nadharia ya Uumbaji walieleza kuwa, kuna majina mengine pia ambayo hupewa watoto wa mwisho kuzaliwa kama vile '*Lyadumila*' na '*Ndumila*'. .

3. ***Njiti*** (mtoto aliyezaliwa na miezi saba): Jina hili hupewa mtoto na wazazi wake ambaye alizaliwa na miezi saba kabla ya kutimiza miezi tisa. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikwa na mtafiti kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa walieleza kuwa, jina hili pia hutolewa kwa kurithi kutoka kwa ndugu wa karibu wa mtoto huyo hata kama hakuzaliwa njiti hii ni kutokana labda kufanana kwa tabia, sura au matendo ya mwanzilishi wa jina hilo ili kuweka kumbukumbu.

4. ***Makutu*** (masikio): Jina hili hutolewa kwa mtoto wa kike au wa kiume ambaye amezaliwa akiwa na masikio makubwa. Wakati mwingine jina hilo hutolewa kwa mtoto ambaye amezaliwa nje ya ndoa kutokana na wazazi wa mtoto huyokutokusikiliza ushauri wa wazazi wao kutokana na tabia ya mama au baba wa mtoto huyo aliyokuwa nayo kabla au baada ya kuzaliwa mtoto huyo.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Makala haya yamewasilisha vigezo vinavyotumika katika utoaji wa majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo ambavyo vimefafanuliwa ni kigezo cha matukio, tabia na matendo ya mtu, mahali pa kuzaliwa, majina ya ujio wa vitu vipya, majina ya wanyama, ndege na wadudu na mahusiano katika familia. Uchanganuzi wa data katika makala haya yameongozwa na Nadharia ya Uumbaji pamoja na mbinu za mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli (maelezo) katika uchambuzi wa data.

**Mapendekezo:** Kutokana na data iliyowasilishwa kuhusu vigezo vya utoaji majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo, makala haya yanapendekeza mbinu mbalimbali za kutumia ili kuendeleza matumizi ya majina ya asili kwa jamii husika kama ifuatavyo: Kwanza, kutoa elimu kwa njia mbalimbali kwa jamii ya umuhimu wa majina ya asili, maana za majina hayo, matumizi yake na hata kujadili umuhimu wa majina hayo ili jamii iendelelee kuyatumia majina hayo. Pili, itolewe elimu kwa vijana na jamii kwa ujumla kuwa majina ya asili yanafumbatia utamaduni, falsafa na historia ya jamii husika. Hii itasaidia mtazamo hasi ya kuwa majina ya asili yamepitwa na wakati yanaweza kuboreshwa kwa kufuata misingi na taratibu za jamii husika kwa lengo la kuendeleza kutunza kumbukumbu na historia ya jamiilugha ya Wagogo. Mwisho, majina haya yanahitaji kulindwa kwa kuwekewa mikakati maalumu ya kuyalinda, kuyahifadhi, kuyatunza, kuyaenzi na kuyaendeleza kwa faida ya kizazi kijacho na taifa kwa ujumla.

**MAREJELEO**


Abel, E. (2012). *Matumizi ya majina ya ukoo katika utambulisho wa jamii ya Wasambaa* (Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).

Anusa, C. A. (2016). *Maana za majina ya watu katika jamii ya Wayao* (Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).

Chulk, O. (1992). *Names from Africa: Their origin, meaning and pronunciation*. John Benjamin Publishing.

Guma, M. (2001). The cultural meaning of names among Basotho of Southern Africa: A historical and linguistic analysis. *Nordic Journal of African Studies, 10*(3), 265–279.

Kofi, A. (2006). The sociolinguistics of Akan person names. *Nordic Journal of African Studies, 15*(2), 206–235.

Koigi, J. (2008). Literary scene: What is in a name. *Daily Nation*, 37.

Matsimela, A. M. (1997). *Sefulediso*. Creda Press.
Mbiti, S. (1990). *African religion and philosophy*. Heinemann Educational Books.
Mekacha, R. D. K. (2011). *Isimu jamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili*. Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Resani, M. (2015). *Semantiki na pragmatiki ya Kiswahili*. Karljamer Print Technology.
Resani, M. (2017). Maana katika majina ya Wabena nchini Tanzania. *Mulika Journal, 44*, 162–196.
Rey, A. (1995). *Essay on terminology*. John Benjamin Publishing.
Rugemalira, J. M. (2005). *A grammar of Runyambo*. University of Dar es Salaam.
Samwel, J. (2016). *Utaratibu wa utoaji wa majina ya asili na maana zake katika jamii ya Wamasai* (Tasnifu M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam).
Sanani, R. M. (2018). *Tathmini ya maana na vigezo vilivyotumika kutoa majina ya utani kwa jamii ya Wapemba* (Tasnifu ya M.A Kiswahili, haijachapishwa, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).
Sapir-Whorf, B. L. (1958). *Language, thought, and reality: Selected writings*. Technology Press of Massachusetts Institute of Technology.
Tegisi, N. M. (2019). *Uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu* (Tasnifu ya Uzamivu, haijachapishwa, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania).
TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. TUKI.